



Itifaki za Kupunguza Maambukizi ya COVID-19 katika Basi ya Usafiri
Lazima familia na wanafunzi wawe macho kwa dalili hizi. Lazima wanafunzi wabakie nyumbani na hawawezi kutumia usafiri ikiwa wana dalili zinazofanana na za mafua, ikiwa mwanafamilia yeyote ana dalili zinazofanana za mafua au amepatikana kuwa na COVID.

1. Wanafunzi wanaelekezwa kukaa kiti kimoja kwa kila mwanafunzi, karibu na dirisha. Lazima wanafunzi wasalie wamekaa na kimya katika safari hiyo ya basi. Wanafunzi wataangalia mbele kwa muda wa safari hiyo na waweke miguu yao kwenye sakafu iliyo mbele yao na mbali na barabara ya basi.
2. Wakati wa kupanda basi, wanafunzi watakaa nyuma ikiangalia mbele na wakati wa kushaka, mbele ikiangalia nyuma.
3. Wanafunzi watapanda au kushuka basi tu katika vituo vyao vilivyoteuliwa.
4. Wanafunzi hawatakataa kukaa katika vitu walivyoteuliwa au kumkataza mtu mwingine kuketi. Viti hivi vimeteuliwa kwa ajili ya kutokaribiana na vimeteuliwa kulingana na mpangilio wa kupanda basi. Wanafunzi watahitaji kukaa kuanzia nyuma hadi mbele.
5. Lazima wanafunzi wavae barakoa kila wakati, isipokuwa kuwe na hali nyingine ya kimatibabu ambayo inaweza kuwazuia kufanya hivyo kwa usalama.
6. Wanafunzi watahitaji kutii kanuni ya maadili mema ya wanafunzi kama inavyohusiana na basi.

Matokeo ya tabia isiofaa kwenye basi ya shule yanayohusiana na COVID19

1. Ripoti ya tabia ndani ya basi huandikwa na kutumwa kwa mwalimu mkuu. Mwalimu mkuu atamuonya mwanafunzi na kutuma nakala ya ripoti hiyo kwa wazazi au walezi wa mwanafunzi.
2. Ripoti ya tabia ndani ya basi huandikwa na kutumwa kwa mwalimu mkuu. Mwanafunzi huamishwa hadi mbele ya basi. Mwalimu mkuu atamuonya mwanafunzi na kutuma nakala ya ripoti hiyo kwa wazazi au walezi wa mwanafunzi.
3. Ripoti ya tabia ndani ya basi huandikwa na kutumwa kwa mwalimu mkuu. Mwanafunzi hunyimwa haki za basi kwa siku tano (5). Mwalimu mkuu atawaarifu wazazi au walezi wa mwanafunzi.
4. Ripoti ya tabia ndani ya basi huandikwa na kutumwa kwa mwalimu mkuu. Mwanafunzi hunyimwa haki za basi kwa siku kumi (10). Mwalimu mkuu atawaarifu wazazi au walezi wa mwanafunzi.
5. Ripoti ya tabia ndani ya basi huandikwa na kutumwa kwa mwalimu mkuu. Mwanafunzi hunyimwa haki za basi kwa muda uliosalia wa mwaka wa masomo au kwa muda wowote unaochukuliwa kuwa unafaa. Mwalimu mkuu atawaarifu wazazi au walezi wa mwanafunzi.

*** Ikiwa mwanafunzi atapoteza haki za basi wazazi au walezi wanaweza kumsafirisha mwanafunzi kwenda na kutoka shule au kumsajili mwanafunzi wao katika masomo ya mtandaoni.**

***Wanafunzi wa Elimu Maalum na Msaada wa Mapema wanaopitia ugumu wataelekezwa kwa mhudumu anayefaa wa mpango (PSE) ili kupanga mfumo wa tabia.**

Saini yangu hapa chini inaashiria Mimi, mzazi/mlezi ninaelewa na nimejadiliana na mtoto wangu kuhusu taratibu za basi na anafahamu matokeo yake. (tafadhali tia saini hapa chini.)

Saini ya Mzazi/Mlezi _____

Tarehe _____

Jina la Mwanafunzi _____

Shule _____

Megan Patton
Mkurugenzi wa
Usafiri wa Wanafunzi

3117 Centre Ave.
Room 366
Pittsburgh, PA 15219

mpatton1@pghschools.org
Simu: 412-529-5947
Faksi: 412-622-5935

Nambari ya wazazi ya Moja
kwa moja:
412-529-HELP (4357)
www.pghschools.org
www.discoverpps.org